# Makutano ya lugha

## Utamaduni na mabadiliko ya kisiasa Tanzania kupitia tawasifu ya Kaluta Amri Abeid
## (The criss-crossing of language, culture and political change in Tanzania through the autobiography of Kaluta Amri Abeid)

*Aldin K. Mutembei*

*Ikisiri:* Kaluta Amri Abedi alikuwa miongoni mwa wahusika muhimu katika maendeleo ya Kiswahili kabla, lakini zaidi, baada ya uhuru. Historia ya lugha ya Kiswahili hasa baada ya uhuru haitaandikwa bila ya kutaja jina la Kaluta Amri Abedi. Majukumu mbalimbali aliyokuwa nayo yanadhihirisha jinsi maisha yake yalivyofungamana na maendeleo na kukua kwa lugha ya Kiswahili. Alikuwa mwanasiasa, msomi na kiongozi wa kidini. Wasifu wake unaonesha makutano ya lugha, utamaduni na mabadiliko ya kisiasa. Ni wasifu unaogusia kwa wakati mmoja changamoto na ushindi wa Kiswahili katika kipindi hiki. Michango ya Abedi ni pamoja na, utetezi wa Kiswahili kama lugha ya taifa, juhudi katika kutafsiri hati za kisheria, kusanifisha lugha ya Kiswahili, na kukuza nafasi yake katika elimu na fasihi. Kujadili wasifu wa maisha yake kunaweza kutoa angalu kidogo, uelewa wa jinsi Kiswahili kilivyobadilika katika mazingira ya kijamii na kisiasa katika Tanzania baada ya uhuru.

*Abstract:* Kaluta Amri Abedi was a key figure in the development of the post-independence Kiswahili. He played a vital role in shaping the social history of the language and made a significant contribution to both religious and political development in Tanzania.

He was a visionary who played a crucial role in the post-independence development of Kiswahili in Tanzania. His work in promoting the language, literature, and culture has had a lasting impact on the nation, helping to shape its social history and national identity. His work was instrumental in shaping the social, cultural, and linguistic landscape of the country, particularly in the context of nation-building and the establishment of Kiswahili as a unifying national language. He was a politician, a scholar and a religious leader. As a Politician he was part of the broader movement led by the Tanganyika African National Union (TANU), the political party spearheaded by Julius Nyerere. Abedi's political activities were closely tied to the nationalist agenda of uniting Tanzanians across ethnic and regional lines. He was a strong supporter of Julius Nyerere's vision of *Ujamaa* (African socialism), which emphasized self-reliance, communal living, and equitable distribution of resources. Abedi's political philosophy aligned with Nyerere's emphasis on using Kiswahili as a tool for social cohesion and national development. He believed that language was a key instrument for mobilizing the masses and ensuring that all Tanzanians could participate in the political and economic life of the nation.

As a religious leader, he was deeply involved in promoting Islamic values and teachings, particularly in the context of Tanzanian society. He used his position to advocate for moral and ethical leadership, emphasizing the importance of honesty, compassion, and social responsibility. As a scholar, Kaluta Amri Abedi's intellectual contributions significantly impacted the development of Kiswahili and Tanzanian culture. His scholarly work was deeply intertwined with his roles as a politician, religious leader, and advocate for national unity. He was a prolific writer and scholar of Kiswahili, contributing to the growth and standardization of the language. He authored numerous books, essays, and poems that enriched Kiswahili literature and demonstrated the language's potential as a medium of intellectual and artistic expression. His advocacy for Kiswahili as a national language was not just a cultural endeavor but also a political strategy to foster unity and collective identity in the newly independent nation. His biography reflects the intersection of language, culture and political changes. Kaluta Amri Abedi was indeed a multifaceted figure in Tanzanian history, known not only for his contributions to the development of Kiswahili but also for his roles as a politician and a religious leader. His work in these areas further underscores his commitment to the social, cultural, and spiritual development of Tanzania Abedi held various leadership positions in local government, where he worked to implement policies that promoted education, healthcare, and rural development. His efforts were particularly focused on improving the lives of ordinary Tanzanians, especially in rural areas. As a politician, he was known for his integrity, dedication to public service, and ability to connect with people from all walks of life. His commitment to social justice and equality made him a respected figure in Tanzanian politics. This article attempts to contextualize the life of Kaluta Amri Abedi within the Tanzania's political, religious and social landscapes.

Maneno ya msingi: Kiswahili; Tawasifu; Utamaduni; Mabadiliko; Uanaharakati.

Keywords: Swahili, autobiography, culture, change, activism

## 1. Utangulizi

Ingawa 'tawasifu' kama somo linalojisimamia halikuwa limevuta umakini wa wanataaluma (Meister 2017), lakini ni uwanja ambao umejaa maarifa na taarifa anuwai. Benton (2007) anaiangalia tawasifu ya mwandishi kuwa ni kazi mseto, inayoonesha historia ya mahali pamoja na simulizi za maisha ya mtu. Benton anaendelea kusema kuwa mwandishi wa tawasifu kupitia uandishi wake, huwasilisha ukweli kama anavyouona yeye katika maisha yake na wakati huo huo huonesha yale yanayotokea kwa nasibu, yale yanayotokeza usumbufu na yale ya kufikirisha, na yote hayo huyafuma katika uandishi mmoja wa

tawasifu ya maisha yake. Msomaji wa tawasifu hutarajia kupata taarifa za hali halisi, zilizofanyiwa utafiti wa kina na kufasiriwa kwa njia ifaayo ili aipate furaha ya kusoma kazi ya sanaa iliyoandikwa vizuri na wakati huo kuipata historia kuhusu jambo fulani.

Katika utangulizi wa Kitabu cha Abedi cha *Almasi ya Afrika: Maisha ya Sheikh Kaluta Amri Abedi* (2010) Sheikh Mubarak Ahmad ambaye alikuwa muumini wa Ahamadiyya kutokea India aliandika waraka kukizungumzia kitabu hicho akisema: "uchapishaji wake utasaidia kueneza taadhima ya Islamu na Ahamadiyyat" (Abedi 2010: v). Hii inatuonesha kuwa kupitia tawasifu ya Kaluta Amri Abedi wasomaji wanaweza kupata taarifa kuhusu mwenendo wa dini ya Kiislamu na kuwapo kwa dhehebu la Ahamdiyya katika Tanzania.

Katika makala hii nimechagua kujadili tawasifu wa Kaluta Amri Abeid kwa kuzingatia vipengele vitatu ambavyo ni lugha ya Kiswahili, utamaduni ambao unaibainisha Tanzania, na mabadiliko ya kisiasa kutoka Tanganyika kuwa Tanzania. Katika makutano ya vipengele hivyo vitatu, ndipo yanapoinukia maisha ya Kaluta Amri Abedi.

Kwa maneno mengine, tutaangalia jinsi lugha ya Kiswahili ilivyojenga na kudhihirisha utamaduni wa mtu mwenyewe na jamii yake. Kisha tutajadili mabadiliko ya kisiasa na ya kijamii na kuyahusisha na maisha ya Kaluta Amri Abedi katika mipaka ya lugha na fasihi ya Kiswahili. Akimwongelea Kaluta Amri Abedi, Sheikh Mubarak Ahmad katika utangulizi wa kitabu kumhusu Kaluta Amri Abedi anasema:

> aliweza kuishinda hali ya kutawaliwa ...wakati huo huo akawa chachu ya maendeleo ya kisiasa, kijamii, kielimu na kiuchumi katika kiwango cha kitaifa (Abedi 2010: vi).

Kwamba Kaluta Amri Abedi 'aliyabadili maisha na mwenendo kwa ngazi ya kitaifa,' inatusukuma kujadili jinsi maisha yake yanavyohusiana na suala la kitaifa. Suala hilo si jingine, bali ni utambulisho wa lugha ya Kiswahili. Kwa hiyo, katika kuyajadili maisha yake tutamchunguza Kaluta Amri Abedi kama Mswahili. Ili kufanya haya, hatuna budi kwanza kumfahamu japo kwa kifupi Kaluta Amri Abedi alikuwa ni nani.

## 2. Kaluta Amri Abedi: kuzaliwa na makuzi yake kuhusiana na lugha ya kiswahili

Kaluta Amri Abedi alizaliwa Ujiji Kigoma mwaka 1924. Alikuwa ni mtoto wa pili wa kiume katika familia ya watoto kumi. Ni vizuri kuangalia hali ya Ujiji ilivyokuwa katika kipindi hiki kuhusiana na Kiswahili ili kuelewa mazingira ya kiisimujamii yaliyomkuza Kaluta Amri Abedi. Akieleza hali ya Ujiji wakati huo McHenry anasema:

> The common language for the people of Ujiji is Swahili and most inhabitants are Muslim. Further, although composed of people from perhaps 30 different tribes, most of those who live in Ujiji do not know their tribal language and have discarded tribal customs. Thus the defining characteristics of 'Swahili Culture' appear to be possessed by the people of Ujiji (McHenry 1973: 405).[1]

Kutokana na hali hii ya Ujiji, tunaweza kufahamu chimbuko la mapenzi aliyokuwa nayo Kaluta Amri Abedi kuhusiana na Kiswahili. Tunaposhuhudia mchango wake katika kukiimarisha Kiswahili hatuna budi kujua kuwa hali hiyo ina usuli wake kutokea katika mizizi ya makuzi yake Ujiji Kigoma. Uchunguzi zaidi katika familia ya Kaluta Amri Abedi unatueleza kuwa kwa asili jamaa yake ilitokea Kongo ya mashariki ambayo leo inaitwa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Baba yake alitokea Kongo ya mashariki katika kijiji cha Karamba. Kujikuta kwake Ujiji ni kwa vile alitekwa na watu ambao hakuwajua na wakampeleka Ujiji Kigoma. Tunaelezwa tu kuwa baba yake alikuwa kutoka ukoo wa kichifu (Abedi 2010). Abedi (2010: 3) anaendelea kueleza kuwa baba yake, Kaluta Amri Abedi, alipenda elimu na moja ya kazi yake wakati wa ukoloni wa Wajerumani na Waingereza ni ya afisa afya ya wananchi akisimamia usafi. Historia kuwa ukoo wa Kaluta Amri Abedi ulitokea Kongo ya mashariki, unaongeza ufahamu wetu kuhusu mapenzi ya Kaluta kuhusiana na lugha ya Kiswahili, moja ya lugha za Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo inayozungumzwa zaidi upande wa mashariki (Kaji 2019; Meeuwis 2006). Kaluta mwenyewe anasema kuwa

> Lugha ya kawaida kwa watu wa Ujiji ni Kiswahili na wakazi wengi ni Waislamu. Zaidi ya hayo, ingawa eneo la Ujiji linajumuisha watu kutoka labda makabila 30 tofauti, lakini wengi ya wale wanaoishi Ujiji hawajui lugha za makabila wanakotokea na pia wameziacha desturi za makabila yao. Kwahiyo, tunaweza kusema kuwa zile kaida, desturi na mila zinazoutambulisha 'Utamaduni wa Kiswahili' walikuwa nazo watu wa Ujiji (McHenry 1973: 405).

## 3. Utabiri kuhusu Kaluta Amri Abedi

Yako mambo mawili tunayoweza kuyazungumzia kumhusu Kaluta Amri Abedi. Jambo la kwanza ni utabiri kuhusu jina lake. Wataalamu wengi walioandika kuhusu nafsi ya jina katika maisha ya Mwafrika. Mbiti (1969), Nyamiti (1988), Igboin (2004), Echekwube (2005), Igboin (2014) kutaja wachache, wanakubaliana kuwa jina huakisi tabia, hulka na maisha ya mwenye nalo. Mbiti (1969) kwa mfano, anasema, kwa Mwafrika, jina huwa na maana. Maana hizo hugusa matukio mengi, hali wakati wa

[1] Lugha ya kawaida kwa watu wa Ujiji ni Kiswahili na wakazi wengi ni Waislamu. Zaidi ya hayo, ingawa eneo la Ujiji linajumuisha watu kutoka labda makabila 30 tofauti, lakini wengi ya wale wanaoishi Ujiji hawajui lugha za makabila wanakotokea na pia wameziacha desturi za makabila yao. Kwahiyo, tunaweza kusema kuwa zile kaida, desturi na mila zinazoutambulisha 'Utamaduni wa Kiswahili' walikuwa nazo watu wa Ujiji (McHenry 1973: 405).

kuzaliwa na jina hilo huathiri utu na tabia ya mhusika ikimaanisha pia huonesha utambulisho wake (Mbiti 1969: 119). Echekwube (2005) yeye anasema kuwa jina si suala la ishara tu, bali pia ni alama inayotuonesha asili, chimbuko, sifa, kazi na mwelekeo wa kitu, mtu au mahali penye jina hilo. Kwa ujumla, jina humpa ubinadamu na asili kwa upande mmoja na kwa upande wa pili huonesha uhusiano uliopo baina ya aliyetoa jina na yule aliyepewa jina.

Wakati mama yake Kaluta, Bi Joha binti Kakolwa akiwa mjamzito, mumewe, yaani baba yake Kaluta alitabiri akisema kuwa atakayezaliwa ni mtoto wa kiume naye atakuwa 'Simba wa Lumona' (Abedi 2010: 9). Abedi anaeleza kuwa jina la Simba wa Lumona, lilikuwa ni la mtemi maarufu huko Kongo aliyetokana na ukoo wa Kifalme. Jina hili lilionesha mtu mwenye kupendwa na watu kwa vile alikuwa na hekima na busara. Imeandikwa kuwa:

> alipoletewa habari za kuzaliwa mtoto wa kiume, [baba yake] alishangilia na kusema: Simba wa Lumona amezaliwa, jina lake ni Kaluta (Abedi 2010: 9).

Jina la Kaluta lilikuwa ni jina la babu yake mzaa baba. Jina lililoonesha heshima kwa mwenye nalo. Tangu wakati huo, makuzi ya Kaluta yalionesha mtoto anayependwa na kupewa heshima kubwa. Baba yake alikaa naye katika vikao vya wazee.Na kila alipopata fursa alimtabulisha kwa wazee wenzake na kila mara baba yake alimtabiria, utabiri wa pili.

Kaluta mpenda elimu. Baba yake alitabiri kuhusu mtoto wake, yaani Kaluta akisema:

> atakuwa bwana wa vitabu na kiongozi. Atakuwa bwana wa wazungu, atakuwa anapaa angani ndani ya mtumbwi (Abedi 2010: 9).

Utabiri kuwa atakuwa bwana wa vitabu ulimaanisha atapenda elimu ya dunia na elimu ya Uislamu. Utabiri huu, ulitokea katika maisha ya Kaluta Amri Abedi kwani mara kadhaa akiwa kiongozi Serikalini alikuwa akisafiri kwa ndege ndogo kutokea Dar es Salaam kwenda Kigoma (Abedi 2010: 10).

Utabiri huo wa 'bwana wa vitabu' ulimaanisha kusoma darasani. Abedi (2010) anaeleza kuwa akiwa na miaka sita tu, Kaluta Amri Abedi alipelekwa katika chuo: akapata elimu ya usomaji. Alisoma shule ya kawaida ya elimu dunia asubuhi, na wakati huo huo jioni alisoma Kuruani Tukufu, Hadithi za Mtume, na Historia ya Uislamu (Abedi 2010; Nawaje 2013). Katika Blog yake, *Kiswahili Jukwaani*, Nawaje Benton anaandika hivi kuhusu elimu ya Kaluta Amri Abedi:

> Baada ya miaka mitatu ya masomo ya Kurani aliingia katika shule ya masomo ya Kizungu. Ujuzi wa lugha ya Kiarabu, elimu ya Madrasa na ile ya kimagharibi ulichangia kumfanya awe mpenzi wa Kiswahili aweze kukizungumza kwa ufasaha. Jambo hili la mapenzi ya Kaluta kwa lugha ya Kiswahili tutalijadili baadaye kwa undani. Baada ya kumaliza elimu ya awali mwaka 1937 alijiunga na Shule

> ya Sekondari Tabora. Baada ya masomo yake ya sekondari Sheikh Kaluta Amri Abed alikwenda kusomea ukarani wa posta Dar es Salaam 1942—1943. Kaluta Amri Abed alikwenda kusoma elimu ya dini Rabwah Pakistan ambako aliweza kufaulu vizuri na kuweza kutunukiwa shahada ya elimu ya dini (Teolojia) (Nawaje 2013; original in a blog in Swahili).

Na kama anayosema yeye mwenyewe Kaluta Amri Abedi, alikuwa amesoma kiasi cha kuweza kutunga mashairi kwa lugha ya Kiingereza, Kiurdu, Kiarabu na Kiajemi (Amri Abedi 1954: ix). Aidha, katika utabiri huo, mwenyewe Kaluta Amri Abedi anasema alianza kutunga mashairi akiwa na miaka kumi na mitatu (Amri Abedi 1954: ix).

Katika makuzi haya, tunaona jinsi utamaduni uliomkuza katika maisha yake Ujiji Kigoma ulimjengea msingi imara katika kupenda kusoma na kupenda kazi. Historia ya familia yake, inaonesha jinsi baba yake mzazi alivyokuwa mwenye maono, hasa kuhusu elimu na uongozi. Baba yake alithamini elimu na alipenda usafi hayo yakamjengea mtoto Kaluta ari ya kupenda kazi na elimu pia. Inaelezwa kuwa:

> mwalimu Hamza Hassan aliongozana na Kaluta Amri Abedi kwenda kwa DC wa Kigoma wa siku hizo, John Rooke Johnson akamueleza kuwa Kaluta Amri Abedi alikuwa ni mwanafunzi mwenye bidii shuleni na katika mtihani wa mwisho alikuwa amekuwa wa kwanza (Abedi 2010: 16).

Kuelewa muktadha wa kitamaduni ni muhimu ili kuufahamu msingi uliomjenga Kaluta Amri Abedi ndani ya mifumo mipana ya kitamaduni na kijamii. Utamaduni wa jamii iliyomkuza Kaluta, yaani jamii iliyoshikilia imani na makuzi ya dini ya Uislamu kwa upande mmoja, na muktadha wa utamaduni kuhusu lugha na hadhi yake katika jamii, yaani jinsi hadhi ya lugha ya Kiswahili ilivyokuwa pale Ujiji ikilinganishwa na hadhi ya lugha nyingine za makabila vilimfanya Kaluta kupenda dini na kupenda lugha ya Kiswahili.

Kwa maneno mengine, elimu ya madrasa (dini ya Uislamu) na ya kimagharibi; na ujuzi wa lugha ya Kiarabu, vilichangia yeye mwenyewe kuwa mpenzi wa Kiswahili na kukizungumza kwa ufasaha. Tunaona kuwa alikuwa mwenye maarifa ya darasani hata akiwa darasa la tisa mwaka 1941 alifanya na kufaulu mtihani wa darasa la kumi (Abedi 2010: 48-49).

Kwa ujumla katika kipengele hiki, huu ni ushahidi kuwa utabiri uliohusiana na jina lake na ule uliohusiana na elimu vilirandana na maisha ya Kaluta Amri Abedi katika uga wa ujuzi wa lugha. Aidha tafsiri ya jina la Simba wa Lumona ilionekana pia katika hedhima aliyoipata katika nyadhifa mbalimbali serikalini. Sehemu ifuatayo inayaangalia maisha ya Kaluta Amri Abedi kama kiongozi wa serikali na kama kiongozi wa dini.

## 4. Kaluta Amri Abedi kama kiongozi

Nafasi ya uongozi wa Kaluta Amri Abedi ilionekana kuanzia alipojiunga na shuleni ya sekondari ya wavulana Tabora. Abedi anaandika: "alikabidhiwa mamlaka ya kuwa msimamizi wa mifugo shuleni. Alikuwa na mamlaka ya uangalizi mzuri wa mifugo ya shule na maziwa yalikuwa yakigawiwa kwa idhini yake" (2010: 17). Kuaminiwa huku na kupewa mamlaka kulichanuza nyota ya uongozi katika maisha ya Kaluta Amri Abedi. Maisha ya kidini, ya kisiasa, ya kielimu na ya kiuanaharakati. Maisha ya mtu aliyekuwa mtetezi katika kila hali. Huu ni utamaduni aliojijengea, na uliomkuza akafanikiwa katika maisha. Maana yetu ya utamaduni inachukuliwa kutoka kwa Hoppenau wanafafanua kuwa utamaduni ni

> Mfumo wa pamoja wa kiimani, maadili, desturi, tabia, na kazi za sanaa ambao hutumiwa na wanajamii katika kukabiliana na dunia na kati ya mtu mmoja na mwingine, na kwamba hurithishwa kutoka kizazi hadi kizazi kwa njia ya kujifunza (Hoppenau na wenzake 2009: 5).

Katika ufafanuzi huu, tunayaona maisha ya Kaluta ya kiimani, maadili, desturi yake a maisha, tabia yake na hata sanaa yake kupitia ushairi wa Kiswahili. Kwa ujumla tunaiona nyota ya uongozi ambayo sasa tunaiangalia hatua kwa hatua katika nafasi zake mbalimbali.

Nafasi za juu za kidini, kisiasa, na kisanaa kutokana na msisitizo kuhusu lugha ya Kiswahili.

Tukiziangalia kazi za Kaluta Amri Abedi tunaona jinsi maisha yake yanavyothibitisha makutano ya lugha, utamaduni na mabadiliko ya kisiasa ya Tanzania. Tunamwona akiwa ndani ya Tanganyika na mchango wake katika mabadiliko ya kuwa nchi huru na kisha kuwa Tanzania.

## 5. Kaluta Mbashiri hadi kuwa Sheikh

Tumekwisha kuona hatua mbalimbali za kidini kutoka kuwa Mbashiri, kwenda masomoni Pakistan na kuwa mwalimu wa dini na Sheikh kamili wa dini ya Uislamu dhehebu la Ahmadiyya. Kupanda kwake hivi katika ngazi za kidini kulikuwa na vikwazo, lakini aliungwa mkono na kupita vikwazo vyote. Alipendwa na washika dini, naye aliwapenda. Alitetewa na washika dini, naye alikuwa mtetezi wao katika nafasi na matukio mbalimbali, iwe katika mikutano au mahakamani. Alitetea dini huku akijenga uhusiano baina ya madhehebu na baina ya dini zote bila ubaguzi.

## 6. Meya wa kwanza Mwafrika wa Jiji la Dar es Salaam

Mwezi Januari mwaka 1960 Kaluta Amri Abedi alichaguliwa kuwa diwani wa Kariakoo. Na baadaye kidogo akachaguliwa kuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam. Hii ilikuwa ni nafasi kubwa kwa Mwafrika.

Tanganyika ilikuwa haijapata uhuru, na ingawa harakati za kudai uhuru zilikuwa zimepamba moto, haikufikirika kuwa 'mapinduzi' yangekuja haraka kiasi hicho, na ikitiliwa maanani kuwa dhehebu lake la Ahamadiyya lilikuwa halina wafuasi wengi kama dhehebu la sunni. Katika kuweka habari zake magazetini, gazeti moja liliandika:

> Mtu maarufu wa wiki[...]ni mshairi aliyebobea, mwanasiasa makini, na mtaalamu wa lugha ambaye aliweza kuzungumza Kiswahili, Kiingereza, Kiurdu, Kiarabu bila wasiwasi wowote (Abedi 2010: 147).

Gazeti hilo la Sunday News la tarehe 24 Januari mwaka 1960, liliweka kwa kifupi wasifu wa Kaluta Amri Abedi. Kwa maudhui ya makala hii, wasifu huo ulieleza makutano baina ya lugha, siasa na utamaduni wa Kaluta Amri Abedi. Utamaduni wake wa unyenyekevu, kuwa mtu wa ibada, kutokuwa na ubaguzi; na kujishusha kunaonekana katika shairi alililoliandika baada ya kuwa meya. Alisema:

> Ujaliwapo makamu, cheo wakakutunuku
> Umeshikishwa hatamu, za punda mwenye shabuka
> Nawe jifanye ghulamu, Kama mtumwa sumbuka
> Kawahudumu kaumu, Khuduma ya kutukuka (Abedi 2010: 149).

## 7. Mjumbe wa Baraza la Kutunga Sheria (LEGCO)

Baraza la kutunga sharia, ama kwa Kiingereza *Legislative Council* - LEGCO, kwa miaka hii ndilo Bunge. Kwa hivi Kaluta Amri Abedi alichaguliwa kuwa 'Mbunge' akiwakilisha 'jimbo' la Kigoma. Itakumbukwa kuwa Kaluta Amri Abedi alikuwa amechaguliwa kuwa mjumbe, kamati kuu ya TANU na mwaka uliofuata yaani 1961, alichaguliwa tena kuwa Meya wa Jiji la Dar es Salaam kwa mara ya pili mfululizo. Katika nafasi hizo mbili, ile ya mjumbe wa Bunge la Kutunga Sharia na ile ya Umeya, Kaluta alidhihirisha pia kuwa si tu alikuwa mwanasiasa makini, lakini pia alikuwa mwanadiplomasia. Alikuwa mwenye uwezo wa kuunganisha watu na kuwa kiungo mwenye uvumilivu baina ya dini tofauti, jinsia tofauti na rangi tofauti. Alikuwa akijaribu kila awezalo kuondoa tabia ya ubaguzi na kujenga udugu na ushirikiano. Kwa mfano wa wazi ni jinsi alivyoshiriki katika bunge la Tanganyika, kwa hotuba ya kizalendo aliyoitoa kuwaeleza wabunge wenzake ubaya wa ubaguzi, huku akiunga mkono sera ya kura ya mseto iliyotaka Waafrika, Waasia na Wazungu wote kukubaliwa kuwa ni raia wa Tanganyika na kuwa na haki sawa kikatiba. Hata kabla yake, alipoalikwa kwenda Marekani, alipewa heshima kuwa raia wa kwanza wa heshima katika mji wa Mansfield (Ohio); jambo ambalo lilikuwa halijafanyika kwa takriban miaka 153 ya historia ya Mansfield (Abedi 2010: 166-167) jambo lililothibitisha kuwa msimamo wake, tabia yake na desturi zake zilikuwa zikiheshimiwa na kukubaliwa hata nje ya Tanzanyika.

Kuwa kwake mkuu wa Mkoa wa magharibi (Tabora ya sasa na Kigoma) kuliendeleza suala la umadhubuti wa uongozi wake kisiasa.

## 8. Waziri wa Sheria na kisha Utamaduni na Maendeleo ya Jamii

Kutoka kuwa mkuu wa mkoa wa Magharibi, Kaluta Amri Abedi aliapishwa kuwa waziri wa sheria wa Tanganyika tarehe 14 Machi, mwaka 1963, akichukua nafasi ya aliyekuwa Waziri wa wizara hiyo, Bw. Abdala Said Fundikira. Na kama mwaka mmoja baadaye, yaani mwezi Aprili mwaka 1964, Kaluta Amri Abedi alichaguliwa kuwa Waziri wa Utamaduni na Maendeleo ya Jamii katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii inayonesha kuwa Kaluta alishiriki katika mabadiliko kutoka Tanganyika na kuwa Tanzania akiwa katika nafasi ya Uwaziri. Alikuwa katika mabadiliko hayo kutokea kwenye sharia na sasa kuingia utamaduni na maendeleo ya jamii. Nafasi zote mbili zina uhusiano na lugha ya Kiswahili. Alishiriki katika kutafsiri Katiba kuwa katika lugha ya Kiswahili na pili, alishiriki katika kujenga na kuimarisha matumizi ya Kiswahili kama urithi muhimu wa utamaduni na tunu ya Mtanzania. Hata alipokuwa Waziri wa sheria, Mwalimu Nyerere, Rais wa Tanganyika hakusita kumwambia:

> Hata hivyo Wizara hii haina mzigo mkubwa. Natumai utatilia pia maanani uboreshaji wa lugha ya Kiswahili (Abedi 2010: 201).

Hii inaonesha kuwa aliongozana na kuambatana na lugha ya Kiswahili katika makuzi na maendeleo yake, iwe katika sanaa ya ushairi, katika tafsiri na hata katika kuikuza kama tunu ya utamaduni.

## 9. Mchango wa Kaluta katika kukua na kuenea kwa Kiswahili

Kutokea utotoni Kaluta Amri Abedi alionesha mapenzi katika lugha ya Kiswahili. Mnyampala (2011) anatueleza kuwa wakati Kaluta Amri Abedi akiwa shuleni darasa la sita, wakati huo anasoma elimu ya Kur'ani, aliwauliza walimu wake

> Kwa nini tunasoma kama Kasuku, hatuelewi yaliyomo katika Aya za Kur'ani tukufu? Kwa nini Kur'ani haitafsiriwi katika Lugha ya Kiswahili (Mnyampala 2011:10).

Ingawa walimu wake Mashekh walimjibu, lakini Mnyampala anatueleza kuwa Kaluta hakuridhishwa na majibu aliyopewa. Kaluta Amri Abedi aliendeleza jitihada za kudai matumizi ya Lugha ya Kiswahili zaidi kuliko lugha zingine. Kwa hiyo, tunapoona baadaye akihariri na kuipitia Kurani iliyotafsiriwa kwa Kiswahili tunaiona dhamira yake aliyokuwa nayo kutokea utotoni ikitimia, yaani kuiona Kur'ani Tukufu ikiwa imetafsiriwa kwa Kiswahili.

Aliipitia na kuihariri tafsiri ya Kurani Tukufu. Kutafsiri Kurani Tukufu kwa Kiswahili juzuu zote thelathini kulifanywa na Sheikh Mubarak Ahmad na kwa kiasi fulani akisaidiwa na Mwalimu Said Kambi kuanzia mwaka 1936 hadi mwaka 1943 ilipochapwa na mashine. Rasimu ya tafsiri hiyo ilipelekwa katika Kamati ya Lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki kwa ajili ya kupitiwa na wataalamu wa Kiswahili na kupata ithibati. Kaluta Amri Abedi aliipitia tafsiri hiyo na kutoa mapendekezo mengi yaliyozingatiwa na Kamati ya Kiswahili (Abedi 2010: 78). Mbali na kujihusisha na tafsiri na uhariri, kwa hakika mchango mkubwa wa Kaluta Amri Abedi katika lugha ya Kiswahili ulikuwa kupitia sanaa ya ushairi.

Kutokea utotoni alikuwa akiimba na kughani mashairi. Kuandika kwake Kitabu cha *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri* (Abedi 1954) ni kielelezo tosha cha umahiri wake katika ushairi. Jambo ambalo lilimpatia nafasi ya kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Ushairi cha Afrika Mashariki. Kazi ya kuandika mashairi na Tenzi na kazi ya kutafsiri nyaraka na miswada mbalimbali kutoka lugha nyingine kuwa katika lugha ya Kiswahili, zilimfanya Kaluta Amri Abedi asiwe, mnenaji tu kuhusu Kiswahili bali mtendaji wa Kiswahili. Alihimiza Kiswahili kwenye dini, alihimiza Kiswahili kwenye elimu na alihimiza Kiswahili kwenye sheria na alitumia Kiswahili kwenye siasa. Mnyampala (2011) anaeleza kuwa katika maisha yake Kaluta alifafanua hoja zake kwa jamii ya Watanganyika na baadaye kwa Watanzania akiwaeleza washairi wa lugha ya Kiswahili pamoja na watumiaji wa lugha ya Kiswahili kukienzi, kukitukuza na kuweka nia njema ya ari thabiti ya kujifunza lugha iliyotukuka lugha ya Kiswahili (Mnyampala 2011: 47). Mnyampala akiendelea kuandika maisha ya mshairi na rafiki yake anasema,

> Katika Mkutano huo Sheikh K. Amri Abedi alichaguliwa kuwa Karii wa chama hicho. Makarii waliochaguliwa siku hiyo walikuwa wanne (Mnyampala 2011: 45).

Kuwa Karii ni sawa na kuwa mhakiki. Mtu aliyeaminiwa katika uga fulani akipewa kazi ya kupitia kukosoa, kusahihisha na kutoa maoni ambayo yalistahili kuzingatiwa na mwandishi wa matini ya awali. Alikuwa Karii wa Mashairi ya Kiswahili—yaani msomaji, mkosoaji na mwelekezaji wa matumizi na maandishi ya lugha ya Kiswahili (Mnyampala 2011: 46). Maisha yake akiwa mtu wa dini, siasa na jamii, akiwa kiongozi katika nyadhifa mbalimbali yalikuwa ni makutano ya lugha na maendeleo ya Kiswahili. Tunaona jinsi lugha iliyomkuza kule Ujiji, aliishikilia na kuitetea katika nyadhifa zake zote. Utetezi huu unatufanya tuangalie jinsi alivyoitumia lugha katika siasa na uanaharakati, kipengele ambacho tunakiangalia katika maisha yake ya kazi.

## 10. Siasa na uanaharakati

Mbali na utetezi katika dini na uhuru wa kuabudu, Kaluta alikuwa mwanaharakati akitetea uhuru wa Tanganyika. Mbali na kuwa kiongozi katika nafasi ya Ustawi wa Jamii, Tabora alijiunga na Tanganyika African Association – TAA na mwaka 1949 alikuwa ni Katibu wake. Abedi anaandika kuhusiana na hili:

> Inaonekana umaarufu huu ukamrahisishia kukubaliwa kuwa mwanachama wa TAA, kwani Hansard report, ya tarehe 27 June 1962, inaonesha kwamba mnamo mwaka 1949 Amiri alishakuwa Katibu wa TAA wa jimbo zima na kuanzisha chama cha kwanza cha wafanyakazi [The Trade Union] hapo Tabora cha 'The Tailor's Association' na mnamo mwaka 1950 aliandaa mgomo wa mafundi cherehani wa Wilaya ya Kigoma (Abedi 2010: 93).

Jambo kama hili bado linarejelea katika jina lake la 'Simba wa Lumona' na utabiri uliotolewa na baba yake kuhusu maisha ya Kaluta Amri Abedi. Kaluta akishirikiana na Bwana Ibrahim Abedi wa Tabora, waliandaa mgomo mwingine wa wa mafundi cherehani wa Tabora ili kudai malipo bora ya kazi yao. Hata hivyo, mgomo huo ulizimwa na Maafisa wa Serikali ya Kikoloni ya Mwingereza baada ya kuizuia pasipoti ya kusafiria ya Kaluta Amri Abedi hadi pale atakapowashawishi mafundi cherehani kuacha mgomo. Alitii, mgomo ukaisha, akaruhusiwa kwena masomoni Pakstani. Kuandaa migomo miwili wa Kigoma na Tabora kulitosha kuwajulisha maafisa wa Kiingereza uwezo aliokuwa nao Kaluta Amri Abedi kwa upande mmoja na ushawishi aliokuwa nao miongoni mwa jamii kwa upande wa pili.

Ukweli huu wa uanaharakati, unatudokezea kwa muhtasari upande wa pili unaomwangalia Kaluta Amri Abedi kama mwanaharakati. Kipengele ambacho tutakijadili kwa undani.

Akiwa bado masomoni, Kaluta alikuwa akiwasiliana na mshairi maarufu Saadan Abdul Kandoro. Alielezwa hatua zote kutoka Tanganyika African Association—TAA hadi kuundwa kwa Tanganyika African National Union—TANU. Katika maelezo ya shairi la '*Siafu Wamekazana,'* Mshairi Saadan Abdul Kandoro aliandikwa hivi:

> Shairi nililiunga kumpelekea marehemu Sheikh K. Amri Abedi alipokuwa kule Missionary College Rabwah Pakistan ili kumjulisha jinsi wananchi wanavyoungana katika kupigania uhuru na kwamba TANU imeundwa (Kandoro 1972: 138).

Kupitia mawasiliano ya kishairi na Saadan Abdul Kandoro, basi Kaluta Amri alikuwa akielewa na kufuatilia kinachoendelea Tanganyika. Msimamo wa Kaluta kuhusu binadamu kuwa huru, ulikwisha kujulikana hasa kupitia shairi lake la mwaka 1953 lililosema *Uhuru jambo halisi, kuukosa ni taabu* (Abedi 2010: 105-107). Hii inatudhihirishia kuwa, maisha ya Kaluta yalishikamana na dini, siasa (kupitia katika ushairi tunaiona pia) na lugha ya Kiswahili.

Yapo japo mambo mawili ambayo serikali ya TANU chini ya Mwalimu Nyerere ilifanya. Mambo hayo yana chimbuko lake katika harakati alizozifanya Kaluta Amri Abedi. Jambo la kwanza ni hotuba kuhusu Kiswahili iliyotolewa na Mwl. Julius Nyerere kwa mara ya kwanza bungeni Disemba mwaka 1962 akiwa Waziri Mkuu wa Tanganyika (Yakubu na Resani 2022: 9). Jambo la pili ni kuhusu Elimu ya watu wazima.

Mambo haya mawili yanaweza kulinganishwa na mafanikio aliyokuwa ameyaonesha Kaluta Amri Abedi. Kwanza Septemba 1951, Kaluta alikuwa ametoa hotuba yenye kichwa 'Kiswahili kitumike katika Baraza la kutunga Sheria' ambapo imeandikwa kuwa mmoja wa wahudhuriaji katika hotuba hiyo Mwingereza aliyekuwa ni Afisa Elimu alipiga kura kuunga mkono hoja iliyotolewa na Kaluta (Abedi 2010: 92). Mapema kabla ya mwaka huo, Saadan Abdul Kandoro alikuwa ameandika shairi mwaka 1948 lenye kichwa cha *Kitumike Kiswahili* akitaka Kiswahili kitumike Bungeni (Abdulrahaman 2020). Kwa hiyo, mwaka 1962, inaposikika hotuba ya Mwl. Julius Nyerere Bungeni kwa Kiswahili tunajua ilikuwa ni hotuba iliyoungwa mkono na washairi, viongozi wa dini na wanasiasa wa wakati huo. Ni hotuba iliyokuwa ikizingatia hali halisi ya siasa na ya kiisimu-jamii kuhusiana na lugha ya Kiswahili.

Aidha, tunaona kuwa baada ya kutoka masomoni Rabwah Pakstan na baada ya kuwa ametoka Tabora na kuhamia Dar es Salaam, Kaluta alianzisha darasa la elimu ya watu wazima katika msikiti wa Mnazi Mmoja. Ingawa masomo yaliyokuwa yakifundishwa kwa watu wazima ni Kiarabu na Kiingereza (Abedi 2010: 116), lakini mafanikio yake yalikuwa ni mbegu iliyozaa wazo lenye kufanikiwa ambapo Mwl. Julius Nyerere alilitumia wazo hilo kuanzisha kwa mafanikio Elimu ya Watu wazima na kuanzishwa rasmi kwa Taasisi ya Elimu ya watu wazima mwaka 1963 (Yakubu na Resani 2022: 9). Kwa hiyo tunayaona maisha ya Kaluta Amri Abed katika dini, siasa, elimu. Alikuwa mtetezi wa wanyonge kwa namna mbalimbali. Tangu waandishi wa habari magazetini (Abedi 2010: 128), kuwatetea viongozi wa kidini (Abedi 2010: 1354-135), na kutetea wanafunzi (Abedi 2010: 135-136). Alitetea wananchi wote bila ya kubaguliwa wapate haki ya elimu. Na kwa utetezi na msimamo wake alichaguliwa pia kuwa Makamu Mwenyekiti wa Tanganyika African Parents Association (TAPA), na mwaka 1959 akachaguliwa kuwa katika Kamati iliyojihusisha na Elimu ya Waafrika. Labda utetezi ambao unaonesha kuwa Kaluta aliwatetea wanyonge, bila ya kujali walikuwa Waafrika ama la, ni mfululizo wa barua alizomwandikia Waziri Mkuu wa India kuhusiana machafuko nchini India mwaka 1947, na mateso na kunyanyaswa kwa wananchi Wahindi wa madhehebu ya Ahmadiya mwaka 1948. Harakati hizi hazikufungamana na dini tu, hata baadaye katika kudai uhuru wa Tanganyika tunamwona Kaluta akiwa ni shupavu, asiyetetereka na mdai haki na uhuru.

Kama tulivyoona kabla, kuchaguliwa kwake kuwa mjumbe wa Baraza la Tutunga Sheria kuwa Meya na baadaye Waziri, kuliithibitisha sauti ya Kaluta kuwa ni mtetezi wa wananchi, mbali na utetezi wake kupitia dini ya Uislamu ya Ahmadiyya.

Jambo la mwisho, ingawa halimo katika uanaharakati, ni suala lake la kupenda michezo. Alipenda michezo, hasa mpira wa miguu akiwa bado kijana mdogo. Alikuwa mchezaji na pia mara nyingi alikuwa mchezeshaji (mwamuzi) wa mpira wa miguu. Ingawa suala hili halijitokezi wazi kama mengine tuliyoyaona, lakini ni sehemu ya maisha yake, na uwanja wa mpira wa miguu wa Arusha kupewa jina lake ni uthibitisho wa mapenzi yake katika kabumbu.

## 11. Hitimisho

Kwa kuangalia maisha ya mtunzi katika nyanja mbalimbali, kwa kufuata maisha ya siasa, dini, elimu na utawala, tawasifu ya Kaluta Amri Abedi imeweza kutumika kama chombo chenye nguvu cha kuangazia masuala ya kijamii na kitamaduni katika Tanzania. Imetumika kuangalia jinsi jitihada za kukuza maelewano, kujenga mazungumzo na kuhamasisha mabadiliko chanya ya kijamii kulivyoijenga Tanzania yenye kuelewana bila ugomvi na machafuko baina ya jamii zenye imani tofauti. Kuunga kwake mkono wakati wa sera ya kura tatu, kunaonesha jinsi kupitia maisha yake suala la ubaguzi lilipigwa vita bila ya kuwapo machafuko.

Kuweka muktadha masuala ya kijamii na kitamaduni ya ukuzaji wa lugha ya Kiswahili kupitia tawasifu ya Kaluta Amri Abedi kumekuwa ni mbinu ya mojawapo ya utambuzi wa vipengele vya kitamaduni vilivyojenga umoja na amani kutokea Tanganyika hadi kuwa Tanzania. Kwa kuweka muktadha masuala ya kijamii na kitamaduni ya mtu binafsi, mchambuzi anaweza kupata uelewa wa kina wa makutano kati ya lugha, utamaduni, siasa, elimu na utawala.

Ni matarajio ya makala hii kuwa kupitia tawasifu, mchambuzi anaweza kuzijadili jitihada za mtu binafsi, changamoto katika maisha na mafanikio katika masuala ya kijamii na kitamaduni huku akiviangalia vipengele vilivyounganika katika ama kuleta changamoto au kusaidia katika kuzikabili. Safari ya maisha kibinafsi ya mtunzi inaweza kuhamasisha wengine ili wajihusishe kwa umakini na vipengele kama vile vilivyoonwa katika tawasifu au vipengele vingine zaidi. Katika makala hii tuliangalia vipengele vya lugha, utamaduni na siasa kama vyenye kufanya makutano katika maisha ya Kaluta Amri Abedi. Tumeangalia muktadha wa kijamii na kitamaduni na jinsi muktadha huo ulivyounda na kujenga uzoefu wa mwandishi wa tawasifu yaani Kaluta Amri Abedi.

## Marejeleo


Abedi, Bakri Kaluta A. 2010. *Almas ya Afrika: Maisha ya Sheikh Kaluta Amri Abedi 1924-1964.* Dar es Salaam: Ahmadiyya Printing Press.

Benton, Michael. 2007. “Reading Biography.” *The Journal of Aesthetic Education* 41(3): 77-88. https://dx.doi.org/10.1353/jae.2007.0023.

Echekwube, Anthony O. 2005. “Good Name and Chieftaincy Titles in Nigeria Today: An Ethical Insight.” In: *Kpim of Morality: Ethics: General, Special and Professional*, edited by Pantaleon Iroegbu and Anthony O. Echekwube, 278-287. London: Heinemann.

Hoppenau, Anna, Johannes Hahn, Olivia Lyimo and Lisa na Bendiek. 2009. *Mwongozo wa Utamaduni. Toleo la Kwanza. Kubadilishana Tamaduni za Kijerumani na za Kitanzania*. Dar es Salaam: Tanzania Youth Coalition na Deutsch Tansanische Partnerschaft.

https://dtpev.de/storage/app/uploads/intranet/public/5bb/46b/e04/5bb46be04d9f4895644632.pdf

Igboin, Benson O. 2004. “Names and the Reality of Life: An Inquiry into Inherent Power in Names among the Owan of Nigeria.” *Ado Journal of Religions* 2: 9-26.

Igboin, Benson O. 2014. “An African Religious Discourse on Names and Identity. Filosofia Theoretica.” *Journal of African Philosophy, Culture and Religions* 3 (1): 26-40.

Kaji, Shigeki. 2019. “How Did Swahili Expand As Far As Eastern Congo? An Account From Its Structural Basis.” *SWAHILI FORUM SPECIAL ISSUE: Variation in Swahili*, edited by Daisuke Shinagawa and Nico Nassenstein. 26: 166-180.

Kaluta, Abedi Amri. 1954. *Sheria za kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* Nairobi: East Nairobi African Literature Bureau.

Kandoro, Abdul S. 1972. *Mashairi ya Saadani*. Dar es Salaam: Mwananchi Publishing.

Khajar, Abdulrahaman M. 2020. “Kuchunguza dhamira za Kijamii katika Mashairi ya Tigiti Sengo: Mfano kutoka katika *Diwani Ya Midulu*.” Tasinifu iliyowasilishwa kwa ajili ya kutimiza sharti pekee la kutunukiwa Digrii ya Uzamili (M.A Kiswahili). Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania. Unpublished Thesis.

Mbiti, Samuel J. 1969. *African Religions and Philosophy*. London: Heinemann.

McHenry, Eugene D. 1973. “A Study of the Rise of TANU and the Demise of British Rule in Kigoma Region, Western Tanzania.” *The African review. A Journal of African politics, development and international affairs* 3(3): 403-321.

Meeuwis, Michael. 2006. “The Lingála-Kiswahili border in north-eastern Congo. Its origins in Belgian colonial state formation of the late nineteenth and early twentieth centuries.” *Africana Linguistica* 12: 113-135.

Mnyampala, Mathias E. 2011. *Historia ya hayati sheikh Kaluta Amri Abedi (1921-1964).* Dar es Salaam: Ahmadiyya Printing Press.

Nawaje, Ali. 2013. “Kiswahili Jukwaani.” Amri Abedi Kaluta (Mshairi Gwiji). Dar es Salaam. https://kiswahilijukwaani.blogspot.com/2013/12/1.html

Nyamiti, Charles. 1988. "The Naming Ceremony in the Trinity: An African Onomastic Approach to the Trinity." *CHIEA African Christian Studies* 4(1): 40-56.

Olatunji, Aabdulganiy, Moshood Issah, Abubakar Muhammed and Abdul Rasheed. 2015. "Personal Name as a Reality of Everyday Life: Naming Dynamics in Select African Societies." *The Journal of Pan African Studies* 8(3): 72-90.

Pantaleon, Iroegbu and Anthony Echekwube (eds.). 2005. *Kpim of Morality Ethics: General, Special and Professional*. Ibadan: Heinemann Educational Books PLC.

Skilleas, Ole M. 2006. "Knowledge and imagination in fiction and Autobiography." *Metaphilosophy* 37(2) DOI.10.1111/j.1467-9973.2006.00423.x : 259-276.

Yakubu, Said and Resani Mnata. 2022. *Mchango wa Mwalimu Nyerere katika Utamaduni, Sanaa, Michezo na harakati za Ukombozi wa Barala la Afrika na Ukuzaji Kiswahili*. Dar es Salaam: Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

Aldin Kai Mutembei (BA Ed.; MA Ling-Dar es Salaam; MA Lit; PhD-Leiden), is the *Mwl. Julius Nyerere* Professorial Chair in Kiswahili at the University of Dar es Salaam. He is the Director of the Institute of Kiswahili Studies, Spokesperson of ACALAN in Tanzania, and the former Director at the Confucius Institute of the University of Dar es Salaam. He teaches Literature, Critical Theories and Oral Literature. His published *Theory of Literary Criticism* is used by scholars in Universities. He is a member of the Board of the Global Association for the Development of Kiswahili in the World, one of the founders of the Association of Kiswahili Teachers in East Africa. His Research Area is in African Literature and Languages, Literary Communication in relation to Community Health and published five books. His PhD (PhD, 2001, Leiden) was about *Poetry and AIDS in Tanzania*. He also researches about the role of African languages in education. He has travelled a lot giving lectures and being a consultant related to Kiswahili and African languages inside and outside Africa. He is an external examiner of African Literature for more than five colleges. He is a member of the Editorial Boards of various Journals. He has written several book chapters and articles published in international journals in Swahili and English languages.

Aldin can be contacted at: kaimutembei@gmail.com